[Namba: 3]

# سُؤَالٌ وَجَوَابٌ

# فِيْ

# أَحْكَامِ الصِّيَامِ

# SWALI NA JAWABU KUHUSU

# HUKUMU ZA SAUMU


**Mtunzi:**

**Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Uthaymin**

**Tarjama:**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

بسم الله الرحمن الرحيم

# FUNGA YA MGONJWA, MSAFIRI NA MWENYE KUSAHAU

## 1- MGONJWA:

**Swali:** Je, kitu gani kinampasa mgonjwa aliyeshindwa kufunga ramadhani?

**Jawabu:** Amesema Allaah Ta'alaa: **[Na atakaekuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hesabu katika siku nyingine]**. **(Surat Al-Baqara/184).** Kwa hiyo tutamwambia mgonjwa huyo: ikiwa yalimpata maradhi halafu amepona, basi ni wajibu juu yake kulipa kwa kufunga masiku yote yaliyompita, kabla ya kuingia ramadhani nyingine. Lakini ikiwa ni ugonjwa wenye kuendelea (kama vile Sukari, Cancer (kansa) Ukimwi (HIV n.k) ambao hautarajiwi kupona kwake, basi atatoa kibaba kimoja kila siku kwa masikini mmoja, wala hatofunga.

**Swali:** Nini hukumu ya kutumia dawa (inayoingizwa tumboni) kupitia njia ya haja kubwa?

**Jawabu:** Hapana ubaya kwa mwenye kufunga kutumia dawa inayoingizwa kupitia njia ya haja kubwa, endapo atakuwa ni mgonjwa, kwa sababu dawa hiyo si chakula wala si kinywaji, wala haijachukua nafasi ya chakula wala kinwyaji.

**Swali:** Je, inaruhusiwa kwa wagonjwa wa pumu kutumia dawa ya kupulizia (Inhaler) mchana wa Ramadhani?

**Jawabu:** Inafaa kwa mwenye kufunga kutumia dawa ya pumu (Inhaler) ambayo (mtu huivuta kwa njia ya mdomo), sawa iwe ni funga ya Ramadhani au siku nyingine, kwa sababu dawa hii haifiki tumboni, bali inafika kwenye mishipa ya pumzi/hewa.

**Swali:** Je, inabatilika funga kwa ajili ya kutumia dawa ya ya kuweka kwenye koo?
**Jawabu:** Hapana, funga haibatiliki endapo atakuwa hajaimeza, lakini ajitahidi mtu asitumie isipokuwa ikiwa hakuna budi, lakini haibatilishi funga muda wa kuwa hajaimeza.

**Swali:** Je, kuchoma sindano kwenye mishipa (kama vile kutoa damu n.k) kunabatilisha funga?
**Jawabu:** Wala mfungaji haitabatilika funga yake kwa kuchoma sindano kwenye mishipa yake au sehemu nyingine (ya mwili wake), isipokuwa ikiwa sindano hiyo imechukua nafasi ya chakula, kiasi ambacho inamtosheleza mtu (sindano hiyo) na kutokula wala kunywa, lakini sindano nyingine kinyume na hiyo haibatilishi funga, ni sawa alichoma kwenye mishipa ya damu au sehemu nyingine.

**Swali:** Je, mtu akitoa damu katika mchana wa Ramadhani kwa ajili ya kupima (kama vile malaria n.k) au kutoa damu ili kumsadia mtu mwingine, atakuwa amefungua?
**Jawabu:** Mtu akitoa damu chache mwilini mwake kiasi ambacho hakuchoka, atakuwa hajafungua, lakini ikiwa ametoa damu nyingi kiasi cha kuwa mwili wake ni wenye kuchoka, basi atakuwa amefungua ni kama vile aliyefanya hijama/kupiga chuku/kuumika.

## 2- MSAFIRI

**Swali:** Ni safari ipi ambayo mtu ameruhusiwa kufungua?
**Jawabu:** Safari ambayo ameruhusiwa ndani yake kufungua na kupunguza swala, ni kilometa (83) na nusu, na kuna miongoni mwa maulamaa hawajaweka kiwango maalumu cha masafa ya safari, bali marejeo ni

matumizi ya wenyeji ya sehemu hiyo, kila masafa ambayo wao huzingatia kuwa safari basi hiyo ni safari. Lakini ikiwa ni kwa ajili ya (kufanya jambo la) haramu, safari hiyo hakuna ndani yake kufungua wala kupunguza swala, kwa sababu haiwezekani kupewa ruhusa kwa ajili ya safari ya kwenda kumuasi (Allaah).

**Swali:** Je, jambo gani bora kwa msafiri, kati ya kufunga au kula (katika mchana wa Ramadhani)?
**Jawabu:** Iliyo bora kwake ni kufanya lililokuwa jepesi kwake, na ikiwa ni sawa kwake kufunga au kula, basi iliyo bora kwake ni kufunga, kwa sababu ndivyo alivyofanya Mtume (Swala na Salamu zimshukie), na kufanya hivyo ni kujiondoa katika dhima (ya kutekeleza ibada kwa haraka) na inakuwa ni wepesi kwa mtu.

**Swali:** Je, kuna masiku maalumu ya kufungua safarini?
**Jawabu:** Hakuna masiku maalumu, kwa sababu Mtume (Swala na Salamu zimshukie) wakati alipoikomboa Makka, aliingia siku ya tarehe 20 na wala hakufunga siku zote (10) zilizobaki.

**Swali:** Ikiwa mtu (amesafiri), mji aliotoka umechelewa kufunga na mji aliokuja umetangulia kufunga, je atafungua wakati gani (ukimalizika mwezi wa Ramadhani?)
**Jawabu:** itamlazimu yeye kufungua pamoja na watu wa mji ule aliokuja, na ile siku iliyopungua kwake atakuja kulipa baada ya kuswali Eid, kadhaalika lau kama alitoka kwenye mji uliotangulia kwenda mji uliochelewa kufunga, basi ataendelea na saumu/funga yake mpaka watapofungua watu wa mji huo.

## 3- SAUMU/FUNGA YA MTU MWENYE KUSAHAU:

**Swali:** Ni ipi hukumu ya mtu aliyekula au kunywa katika (mchana wa Ramadhani) kwa kusahau, na atafanya nini endapo atakumbuka wakati huohuo?

**Jawabu:** Mwenye kusahau (akala au akanywa) funga yake ni sahihi, hata kama atakula sana na atakunywa sana, lakini ni wajibu wake kujizuia kula na kunywa pindi tu akikumbuka, hata kama tonge (la chakula) au kinywaji kipo kinywani mwake, basi atakitema, kwa sababu udhuru (wa kusahau) tayari umeondoka.

**Swali:** Endapo mtu amefunga, akaonekana anakula au anakunywa katika mchana wa Ramadhani, je atakumbushwa au ataachwa bila kukumbushwa?

**Jawabu:** Mtu atakaemuona mfungaji anakula au anakunywa mchana wa Ramadhani, basi ni wajibu wake amkumbushe, na inapasa kwa mfungaji (akikumbushwa) ajizuie na kuacha kula.

**********************************

## FAIDA KATIKA NAMNA YA KULISHA MASIKINI:

Mtu amepewa hiyari ya kutoa kila siku nusu ya pishi, (pishi ya Mtumeﷺ) kumpatia masikini mmoja hali ya kuwa ni fidia yake kwa ajili ya kushindwa kufunga saumu ya ramadhani, atatoa chakula kinacholiwa na kupendwa sana katika mji, au atapika chakula na kuwatosha masikini kwa idadi ya siku ambazo hakufunga, nusu ya pishi ni sawa na kilo moja na robo kwa vipimo vyetu, na hapa inakusudiwa pishi ya Mtumeﷺ ambayo ni sawa kilo mbili na nusu, kwa sanadi sahihi kutoka kwa Zaid bin Thabit رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

**Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah**
**16/sha'bani/1444H – 8/3/2023M**
**Pongwe Tanga.**